



# JARIDA LA USHIRIKA



ISSN 2714 - 2175

Toleo Na: 010

Aprili - Juni, 2022



## NITAULINDA USHIRIKA KWA KUWA NDIYO MFUMO WA KUMKOMBOA MNYONGE - WAZIRI BASHE



***"Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi"***

## YALIYOMO

KUTOKA KWA MRAJIS	<b>02</b>
NITAULINDA USHIRIKA KWA KUWA NDIYO MFUMO WA KUMKOMBOA MNYONGE - WAZIRI BASHE	<b>03</b>
KAMATI YA BUNGE YAIPONGEZA SERIKALI KUANDAA MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA	<b>04</b>
TUNAENDA KUWA NA USHIRIKA WA KUZALISHA UTAJIRI - NAIBU WAZIRI WA KILIMO	<b>05</b>
TANZANIA NA BURUNDI ZABADILISHANA UZOEFU KUHUSU USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA	<b>07</b>
VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA SHINYANGA WAPATIWA MAFUNZO YA UONGOZI	<b>07</b>
MKOA WA SIMIYU KUFUFUA VIWANDA VYA USHIRIKA VYA PAMBA	<b>08</b>
WATOA HUDUMA WATAKIWA KUTOKUSHAWISHIWA NA RUSHWA	<b>08</b>
WANAUSHIRIKA WAASWA KUENDESHA USHIRIKA KIUSHINDANI NA KIBIASHARA	<b>10</b>
VYAMA VYA USHIRIKA VYA WANAWAKE KUANZISHWA MKOANI GEITA	<b>11</b>
WAJUMBE WA BODI MKOANI TABORA WAPATIWA MAFUNZO YA USIMAMIZI WA VYAMA	<b>12</b>
WAANDISHI WASHINDA TUZO ZA UANDISHI WA HABARI ZA USHIRIKA	<b>13</b>
MAAFISA USHIRIKA WAKABIDHIWA PIKIPIKI KUTOKA TCDC	<b>14</b>
NAIBU WAZIRI WA KILIMO AWATAKA WASIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA KUIMARISHA MIFUMO YA USIMAMIZI	<b>15</b>
WANAWAKE WATAKIWA KUJIUNGA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA	<b>15</b>
KONGAMANO LA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA LAFANYIKA TABORA	<b>16</b>
MCHAKATO WA UANZISHWAJI BENKI YA USHIRIKA UFANYIKE MAPEMA - DKT. ISHENGOMA	<b>17</b>
TUME YA USHIRIKA NA BENKI YA NMB ZAINGIA MAKUBALIANO UJENZI WA MAGHALA KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA	<b>18</b>
TCDC NA FSDT ZAINGIA MAKUBALIANO KUIMARISHA VYAMA VYA USHIRIKA	<b>19</b>
VIONGOZI WA USHIRIKA WATAKIWA KUWA WAAMINIFU NA MADHUBUTI	<b>20</b>
VYAMA VYA USHIRIKA DAR-ES-SALAAM VYAOMBA KUPUNGUZIWA KODI YA MAPATO	<b>21</b>
SERIKALI YAKIKABIDHI KIWANDA CHA MANONGA GINNERY KWA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA IGEMBENSABO	<b>22</b>
JIFUNZE KUTOKA CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO USALAMA WA RAIA (URA SACCOS)	<b>23</b>
UJUMBE WA USHIRIKA KIPITIA VIBONZO ( KATUNI)	<b>28</b>

## KUTOKA KWA MRAJIS

### Ndugu Wasomaji,

Niwakaribishe tena katika Jarida la Ushirika, Toleo la Kumi, ambalo ni mfululizo wa majarida yanayoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika jitihada za kuelimisha na kuhamasisha umma kuhusu masuala na hatua mbalimbali zinazofanyika katika kuimarisha Sekta ya Ushirika..

### MANUFAA YA MAADHIMISHO YA SIKU YA USHIRIKA DUNIANI

Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani kwa Mwaka huu yamefanyika kitaifa mkoani Tabora kuanzia tarehe 28 Juni -02 Julai, 2022 na kukutanisha Viongozi wa Ushirika wakiwemo wa Vyama vya Ushirika, Wadau wa Ushirika na Viongozi wa Serikali wanaosimamia Sekta ya Ushirika. Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Ushirika Hujenga Ulimwengu Bora' Maadhimisho haya hufanyika vilevile katika ngazi ya mkoa (Jukwaa la Ushirika) na kilele chake hufanyika kitaifa kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi Julai.



Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).

Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani husaidia kutangaza mafanikio kwa umma yatokanayo na kazi za wanaushirika, kuhabarisha umma juu ya falsafa na manufaa ya Ushirika na hutoa fursa ya kujadili changamoto mbalimbali za kiuchumi na kijamii zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi.

Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani husaidia kuwaunganisha wanaushirika na wabia wa

maendeleo toka ndani na nje ya nchi na husaidia kuvunganisha Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kuimarisha mahusiano katika kusaidiana kwa masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani husaidia washiriki mbalimbali kupata fursa za kielimu sambasamba na kubadilishana uzoefu kuitia makongamano mbalimbali wakati wa maadhimisho na hutoa fursa kwa Vyama vya Ushirika na Wadau wa Maendeleo ya Ushirika kubadilishana uzoefu, mbinu za usimamizi, ubunifu na mtandao wa masoko.

Kuitia maadhimisho haya Vyama Vya Ushirika, wadau wa Sekta ya Ushirika na taasisi za Serikali huonyesha bidhaa na huduma zinazotolewa na taasisi hizo kwa wananchi na wakulima wanaotembelea ili kuwawezesha kujifunza kwa vitendo kwa kujionea kazi mbalimbali za wanaushirika na wadau wake.

Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani hutoa fursa kwa washiriki kutekeleza msingi wa ushirika wa kuijali jamii kwa washiriki wote kushiriki katika utoaji wa misaada na mahitaji kwa wahitaji kama vile Yatima, wagonjwa hospitalini; ushiriki katika upimaji afya na uchangiaji damu pamoja na masuala ya michezo.

Vilevile, Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani hutoa fursa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kutoa huduma kwa washiriki na kupelekea kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, uchumi wa mkoao husika na taifa kwa ujumla; na hutoa fursa kwa wadau wa maendeleo ya Ushirika kujifunza kuhusu fursa za uwekezaji na ufanyaji biashara kuitia mazao na bidhaa yanayozalishwa kwenye Vyama vya Ushirika.

Ni kutokana na manufaa ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani, tunawaasa Wanaushirika na Wabia wa Maendeleo toka ndani na nje ya nchi kushiriki kikamilifu kuonyesha bidhaa na huduma zinazotolewa katika Vyama vya Ushirika na Wadau wake.

## NITAULINDA USHIRIKA KWA KUWA NDIYO MFUMO WA KUMKOMBOA MNYONGE - WAZIRI BASHE

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, amesema ataulinda na kuutetea Mfumo wa Ushirika popote atakapokuwa kwa kuwa ndiyo mkombozi kwa watu wanyonge.

Mhe. Bashe amesema hayo wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) kwa mwaka 2022 yaliyofanyika mjini Tabora kwa siku tano kuanzia tarehe 28 Juni, 2022 hadi leo tarehe 02 Julai, 2022.

"Nitaulinda na kuutetea Ushirika popote pale kwa kuwa ndiyo mkombozi wa Mtu mnyonge, awe mkulima au Mjasliamali yeyote; Ushirika kama Mfumo hauna matatizo, tatizo ni baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Ushirika," alisema Mhe. Waziri.



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe akizungumza na Wanaushirika katika Maadhimisho ya SUD - 2022*

Mhe. Waziri Bashe amewataka Wanaushirika kuchagua Viongozi mionganoni mwa Wanaushirika wenyewe, wakiwemo wakulima wanaouza mazao yao kwenye Vyama vya Ushirika. Wanaochaguliwa lazima wawe wabunifu na waaminifu.

"Kama Mimi ni mkulima nipewe haki ya kuchaguliwa, kuchagua Viongozi ninaowataka

na kupata taarifa kwenye Chama changu cha Ushirika," amesema Waziri Bashe.

Vilevile, Mhe. Bashe amesema Serikali imedhamiria kutengeneza taasisi ya fedha ambayo itatunza fedha za Wanaushirika wakiwemo wakulima na wajasliamali wengine; Taasisi hiyo ni Benki ya Taifa ya Ushirika.

"Benki ya Ushirika itatumika kama jukwaa la Majadaliano kati ya Wanaushirika na taasisi za fedha na kuwawezesha wanaushirika kupata faida kwenye akiba wanazoziweka kwenye Benki hiyo," amesema Waziri.

Aidha, Waziri Bashe amesema Serikali imedhamiria kufufua ginery za kuchambua Pamba zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika ili kuongeza thamani ya zao la Pamba na mazao yake.

"Lazima tuenze Safari ya Kuongeza thamani ya mazao yetu, tuchague Viongozi amba ni Wanaushirika wenzetu na wenyewe uchungu na Mali za Ushirika," ameeleza Mhe. Bashe.



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe akitembelea mabanda ya Wanaushirika katika Maadhimisho ya SUD - 2022*



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe akitembelea mabanda ya Wanaushirika katika Maadhimisho ya SUD - 2022*



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege (kulia) akikabidhiwa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe ufunguo wa Pikipiki kama ishara ya kukabidhi pikipiki nane (8) zilizotolewa na Benki ya CRDB zitakazotumiwa na Warajis Wasidizi wa Mikoa kwa ajili ya usafiri.*

## KAMATI YA BUNGE YAIPONGEZA SERIKALI KUANDAA MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imeipongeza Serikali kuitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kuaandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Waheshimiwa wabunge wa Kamati hiyo wamesema matumizi ya Mfumo huo yatasaidia kuboresha huduma zinazotolewa kwa Wanaushirika kuitia Vyama vya Ushirika Nchini.



*Mhe.Dkt. Christine Ishengoma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji akizungumza kwene kikao hicho*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliwasilisha Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika unaoandaliwa kwa Kamati Mei 10, 2022, Jijini Dodoma ili kupata maoni yao kabla ya kuanza matumizi ya Mfumo huo.

Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, amesema kuwa Maoni na Ushauri uliotolewa na Wabunge utafanyiwa kazi kabla ya Mfumo kuanza kazi.



*Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, akizungumza katika kikao hicho*

## **TUNAENDA KUWA NA USHIRIKA WA KUZALISHA UTAJIRI - NAIBU WAZIRI WA KILIMO**

Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Antony Mavunde, amesema kutohana na Tafiti zinazofanyika kwenye Sekta ya Ushirika, sasa Ushirika unaenda kuwa wa kuzalisha utajiri na sio migogoro na matatizo.

Naibu Waziri Mavunde ameyasema hayo tarehe 12/05/2022 kwenye ufunguzi wa Kongamano la Pili laTafiti za Ushirika lilioandaliwa na Tume ya maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi (MoCU).

Mhe. Naibu Waziri amewataka Wanaushirika kwenda kubadili picha na mtazamo wa Ushirika na si kubaki kukazana na yale yale mambo mabaya kila siku ambayo yameendelea kuurudisha nyuma Ushirika.

"Ushirika huu una uwezo wa kuwa na mchango mkubwa kwenye ustawi wa taifa letu la Tanzania, tunaweza kupiga hatua kwa kujiunga kwenye Ushirika," amesema Mheshimiwa Mavunde.

"Ukiangalia fursa mbalimbali zilizopo nchini, kama upatikanaji mafuta ya kula; Kuna uhitaji wa Tani Laki Sita na elfu hamsini kwa mwaka na uwezo wa ndani wa kuzalisha ni Tani laki mbili na tisini elfu tu, inailazimu Serikali kuagiza mafuta ya nje yenye thamani ya billion 474. Kwahiyoo kupitia Kongamano hili twendeni na tuje na suluisho la kuisaidia Serikali," amesema Mhe. Mavunde



Baadhi ya Washiriki wa Kikao hicho cha Warajisi Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa na Menejimenti ya TCDC

Aidha, Mhe. Mavunde amewapongeza Wanaushirika kwa kuafiki na kuanzisha Mfuko kwa ajili ya Tafiti, na kuridhia kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika.

Awali, Mrasis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC), Dkt. Benson Ndiege amesema, kongamano hilo ni muhimu katika kuibua changamoto za Ushirika na kuzitafutia ufumbuzi. "Tunachotakiwa hapa ni kuibua changamoto na kuziwekea utekelezaji kwa akili ya mwaka unaokuja." amesema Dkt. Ndiege.

Akitoa maelezo ya kongamano hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya kongamano hilo, Dkt. Edmund Zakayo, amesema wameamua

kufanya makongamano ya tafiti za Ushirika kutokana na tafiti nyingi kutokuwa na tija kwa kuwa zinaandaliwa na kuandikwa kwa lugha ya kiingereza, ambayo siyo rafiki kwa baadhi ya Wanaushirika.

Amesema, hali hiyo imefanya tafiti hizo kubaki kwenyemakaratasi kutokana na lugha inayotumika katika kuziandaa na kutokusambazwa kwa walengwa. "Kutokana na hali hiyo ikaonekana umuhimu wa kuandaa kongamano la kwanza la tafiti za Ushirika na hatimaye kuazimia kuwa na kongamano kila mwaka ili tuweze kupata fursa ya kujadiliana matokeo ya tafiti na namna ya kutatua changamoto zilizopo katika Sekta ya Ushirika." amesema Dkt. Zakayo.



Wanaushirika wakiwa katika Kongamano la Pili la Tafiti za Ushirika

## TANZANIA NA BURUNDI ZABADILISHANA UZOEFU KUHUSU USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Ujumbe wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) umefanya Ziara ya kikazi Nchini Burundi, Aprili 11, 2022 na kufanya Kikao na wenyeji wao ambapo Mamlaka ya Uthibiti wa Vyama vya Ushirika Burundi (ANACOOP) waliwasilisha namna wanavyosimia Vyama vya Ushirika na TCDC iliwasilisha Majukumu yake, na baadaye kubadilishana uzoefu. Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Mhe. Balozi Dkt. Jilly Maleko, alihudhuria kikao hicho.



*Ujumbe wa Tanzania katika ziara hiyo uliongozwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege (wapili kushoto mbele)*

Aidha, Ujumbe wa Tanzania ulitembelea Vyama vya Ushirika Nchini Burundi ili kujionea Mafanikio katika Sekta ya Ushirika na kujifunza namna nchi hizo zitakavyoweza kushirikiana na kuwanufanuisha Wanaushirika wa pande zote mbili.

## VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA SHINYANGA WAPATIWA MAFUNZO YA UONGOZI

Serikali ya Mkoa wa Shinyanga imewataka viongozi wa Vyama vya Ushirika kuwa waaminifu katika kulipa wakulima bei stahiki na kujitahidi kudhibiti ubora wa mazao, usafi wa mazao na vipimo sahihi wakati wa kuuza mazao ili yaweze kupata bei nzuri.

Hayo yamesemwa Aprili 28, 2022 na Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika (Madini, Pamba na Tumbaku) Mkoa wa Shinyanga yenye lengo la kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya usimamizi wa Ushirika, kuijiendesha kibashara na Maadili ili waweze kufanya shughuli zao vizuri.



*Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary akifungua mafunzo ya siku mbili kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika mkoani Shinyanga*

Ommary ameshauri pia mazao yaliyopo kwenye Ushirika ambayo ni Pamba, Korosho, Mkonge na Tumbaku yapangwe katika madaraja sahihi ili kumrahisishia mnunuzi kutoa bei nzuri zaidi kuliko kuchanganya.

"Hivi sasa tunaelekea msimu wa masoko kwa mazao ya Pamba na Tumbaku. Niwaombe tujaribu kusimamia masoko yetu vizuri ili kuhakikisha changamoto za msimu uliopita hazijirudii. Tuweke mifumo mizuri ya uuzaaji na ulipwaji wa pesa zetu hasa upande wa vyama vya pamba, tuachane na malipo ya pesa taslimu yatatusheweshea maendeleo na kutusababishia migogoro ya upotevu na wizi wa pesa za pamba," amesema Ommary.

Aidha, amewahimiza Wanaushirika kuunga mkono juhudzi za Serikali kwa kufanya kazi kwa bidii na kulima kilimo chenyetija na kilimo cha kisasa na kuachana na kilimo cha mazoea, kwani serikali inaendelea kutoa fursa mbalimbali za kumkomboa mkulima ikiwemo kutoa dawa na mbegu bure, kuboresha huduma za ugani kwa kugawa vitendea kazi kwa Maafisa Ugani nchi nzima na benki kupunguza riba kwenye kilimo.

Katika hatua nyingine amevitaka Vyama vya Ushirika kuhakikisha vinachagua viongozi wenye uwezo wa kufanya kazi kwa misingi ya Utawala Bora badala ya kufanya kazi kwa mazoea huku akisisitiza kuwa viongozi hao wanatakiwa kuwa

wenye maono, wabunifu na kuweza kuzitunza na kuzilinda mali za wana ushirika na siyo kuhujumu mali hizo.

Naye Mrasis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, amesema mafunzo hayo kwa Wajumbe wa bodi yanatarajiwa kuleta tija kwa kuonesha mabadiliko chanya kwa viongozi wa vyama vya ushirika katika maeneo wanayoyasimamia.

"Mafunzo haya yana lengo la kukumbushana wajibu na mipaka ya vyama vya ushirika, kubadilishana mawazo, kuwakutanisha na wadau wa sekta ya kilimo ili kuonesha fursa zilizopo kwani tunataka kuhakikisha vyama vya ushirika vinakuwa endelevu," alisema Boniphace.

"Tunataka Ushirika uwe imara na ujiendeshe kibiashara. Tunashukuru viongozi wa vyama vya ushirika wamehudhuria mafunzo haya kwa wingi tofauti na matarajio yetu hii inaonesha ni kiasi gani wanataka mabadiliko katika kuboresha utendaji kazi wao," amesema Boniphace.

Mkoa wa Shinyanga una jumla ya vyama vya Ushirika vya Msingi 457 vyenye jumla ya wanaushirika 46,395. Pia kuna vyama vya Upili vitatu vinavyojumuisha Union mbili za SHIRECU LTD na KACU LTD. Pia, Mkoa una jumla ya SACCOS 7 ambazo zimepata leseni kati ya SACCOS 20 zilizopo katika Mkoa mzima.



Viongozi wa Vyama vya Ushirika Mkoani Shinyanga wakila kiapo cha kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria

## MKOA WA SIMIYU KUFUFUA VIWANDA VYA USHIRIKA VYA PAMBA

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. David Kafulila, amesema Serikali ya Awamu ya sita chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, imetenga kiasi cha Shilingi Billion sita (6) kwa ajili ya kufufua Viwanda vya Pamba Mkoani Simiyu.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. David Kafulila akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Simiyu

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu amesema kuwa kufufuliwa kwa viwanda vya Pamba vinavyomilikiwa na Ushirika kutachochea kufanya vizuri kwa zao la Pamba katika Ushirika kwa msimu huu baada ya kuzitatau changamoto zote zilizokwauwa zao hili.

Mheshimiwa Kafulia ameyasema hayo katika Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Simiyu (SIMCU) uliofanyika jana tarehe 05/04/ 2022, Mjini Bariadi.

"Sisi tunaongoza kwa Pamba hapa Tanzania, Vyama vyetu vya Ushirika vikijisimamia kuanzia ngazi ya msingi na vijiji vitaimarika kutoekana na usimamizi wa mauzo ya Pamba kupitia Mfumo wa Ushirika," amesema Kafulila.

Akizungumza katika Mkutano huo, Mrasis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Dkt. Benson Ndige, ametaka uongozi mpya utakaochaguliwa kwenda kusimamia maslahi ya wakulima wa zao la Pamba kuепuka tuhuma mbalimbali zinazoelekezwa kwa baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Ushirika kutokuwa waadilifu.

Aidha, Mrasis ameshauri kuwa watendaji katika ngazi ya Karani na Wahasibu kuajiriwa wanaotoka ndani ya Mkoa husika kuепuka Chama kuibiwa na kukimbiwa mara kwa mara.

Mkutano Mkuu wa SIMCU uliambatana na uchaguzi wa Viongozi wa Bodi mpya ya Chama Kikuu cha Ushirika SIMCU, baada ya Bodi iliyokuwa madarakani kumaliza muda wake.

Viongozi wapya wa Bodi ya SIMCU waliochaguliwa ni Mwenyekiti, Lazaro Walwa, Makamu Mwenyekiti, Kulwa Bupuna na Wajumbe ni Makoye Bwile, Philimon Sambe, Susan Masanja, Simon Magoma na Shiboka Petro. Mwakilishi ni Jenipha Emanuel.

## WATOA HUDAUMA WATAKIWA KUTOKUSHAWISHIWA NA RUSHWA

Watoa Huduma katika Vyama vya Ushirika wametakiwa kutoa huduma kwa uwazi na ufasaha mkubwa pasipo kushawishiwa na vitendo vya rushwa; na kwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika.

Wito huo umetolewa na Mrasis wa Vyama vya ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndige alipofungua Kikao Kazi cha TCDC na Watoa Huduma katika Vyama vya Ushirika kilichofanyika Jijini Dodoma, Aprili 06, 2022.

"Kwa kuwa Serikali imeweka Imani kubwa kwenu ili kuvihudumia Vyama vya Ushirika ambavyo ni vyombo vya wananchi wake ambao wengi wao

ni Wakulima. Toeni huduma zenu kwa uwazi na ufasaha mkubwa pasipo kushawishiwa na vitendo vya rushwa" amesema Dkt. Ndige.



*Mrajis wa Vyama vya ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndige akifungua Kikao Kazi cha TCDC na Watoa Huduma*

Mrajis amewataka Watoa Huduma kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya Ushirika na uendeshaji wake na kufuata Misingi ya Ushirika inavyoelekeza.

"Hakikisheni kuwa huduma zenu zinatolewa kwa wakati stahiki kulingana na mikataba yenu na Vyama. Mfano, wakati mmekubaliana kukusanya madeni au kufunga mtandao wa TEHAMA, hakikisheni huduma hizo zinatolewa kwa wakati na sio kuachia kazi njiani," amesema Dkt. Ndige.

Aidha, Mrajis amewataka Watoa Huduma katika kutekeleza majukumu yao kwa Vyama vya Ushirika kuhakikisha kuwa wanashirikiana na Warajis Wasaidizi na Maafisa Ushirika waliopo katika maeneo husika ili kuimarishe udhibiti wa huduma wanazozitoa kwa Vyama vya Ushirika, na pia kuweza kutambulika.

"Vyama vyetu vya Ushirika viro katika maeneo mbalimbali yaani mijini na vijiji, na wote hawa ni Watanzania ambao wanatamani vyombo vyao vipige hatua ya kimaendeleo. Hivyo hamna budi kuhakikisha kuwa hamfungamani pekee na aina fulani ya vyama vya ushirika mfano SACCOS zilizopo mijini pekee mkasahau zile za vijiji. Toeni huduma zenu pasipo upendeleo," amesema Mrajis.

## WANAUSHIRIKA WAASWA KUENDESHA USHIRIKA KIUSHINDANI NA KIBIASHARA

Mkutano Mkuu wa Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya Pamba (Tanzania Cotton Co - Operatives Joint Enterprise Limited - TANCCOOPS LTD) umefanyika Mei 05, 2022 Mkoani Shinyanga huku wajumbe wa mukutano huo wakiaswa kujisimamia na kuendesa Ushirika kiushindani na kibashara.

Mkutano Mkuu wa TANCCOOPS LTD umefanyika katika ukumbi wa mikutano wa SHIRECU na kuhudhuriwa na wajumbe wa TANCCOOPS LTD inayoundwa na Vyama Vikuu vya Ushirika 14 kutoka kwenye Mikoa inayolima zao la Pamba.



*Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika nchini (TFC), Charles Jishuli akizungumza kwenye mukutano huo*

Mbali na kujadili masuala mbalimbali ya kuimarishe Ushirika, Mkutano huo pia umeenda sanjari na Uchaguzi wa wajumbe wa bodi na mwakilishi nje ya bodi ya TANCCOOPS LTD ili kuziba nafasi zilizokuwa wazi ambapo Baraka Joseph Masoko - kutoka Mirambo Union na Lazar Kidiga Walwa wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Bodi, na Daniel Mwita Masanja akichaguliwa kuwa Mjumbe nje ya Bodi baada ya kupigwa kura na wajumbe 17 wa mukutano.

Msimamizi wa uchaguzi huo, kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa niaba ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Grace Mwangende amesema mchakato wa uchaguzi umefanyika vizuri huku akisisitiza kuwa endapo mjumbe wa Bodii atakayekengeuka mbele ya safari atakaa nje na nafasi yake kujazwa na mjumbe mwengine.

"Naomba Wanachama muwe na uchungu na chama ili kujenga ushirika na TANCCOOPS LTD kuwa imara zaidi. Tasnia ya pamba inavyokwenda mnatakiwa mijikaze zaidi, na muifanye kibiashara," amesema Mwangende.

Mwangende amesisitiza kuwa Ushirika ni biashara hivyo kuwataka viongozi wa vyama vya ushirika kuwa wabunifu wanapoongoza wenzao.



*Grace Mwangende, Mwakilishi wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kutoka TCDC akizungumza katika mkutano huo*

"Ninawaomba msiuchukulie ushirika kama pori, msijifanye wajuaji sana kwenye vitu msivyovifahamu mkaharibu mambo. Tunataka Ushirika biashara. Naomba pia mhamasishé wanawake waingie kwenye ushirika kwani walipo ni wachache sana," amesema Mwangende.

Naye Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoo wa Shinyanga, Hilda Boniphace, aliyekuwa Mgeni Rasmi katika Mkutano huo amesema Ushirika ni ushindani hivi sasa, hivyo ni lazima Ushirika ujiendeshe kibiashara ili kuepuka kuchafuka.



*Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoo wa Shinyanga, Hilda Boniphace, akizungumza na Wanauushirika*

"Shindaneni kiushirika badala ya kutafuta pa kutupiana lawana ama kulalamika tu. Vyama vya Ushirika sasa viache kufanyabkazi kwa mazoea kwasababu ushirika ni kama private sekta na kwa kuwa tunafanya biashara ya mazao ya kilimo na kuongeza thamani, basi lazma Ushirika ujipange kukabiliana na ushindani wa biashara. Na kutumia fursa zilizopo kufanya maajabu na kuurudisha Ushirika kwenye reli," amesema Boniphace.

## VYAMA VYA USHIRIKA VYA WANAWAKE KUANZISHWA MKOANI GEITA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imeratibu na kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Wanawake Mkoo wa Geita tarehe 05.05.2022 kwa lengo la kuhamasisha Wanawake ambao ni wajasiriamali, wafanyabiashara, wafugaji, wavuvi, wasusi, washonaji, Mafundi, wakulima na wazalishaji kwenye shughuli nyingine za kiuchumi kujiunga pamoja na kuanzisha Vyama vya Ushirika utakaokuwa 'multipurpose' kwa kutumia 'MADIRISHA Business Model.'



Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege akizungumza na washiriki wa Mkutano wa Jukwaa la Wanawake Mkoa wa Geita

Lengo la Serikali kuitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika ni kuimaraisha Sekta ya Ushirika na kuboresha maisha ya wananchi wake kwa ujumla kwa kuitia makundi mbalimbali kama wanawake, vijana na watu wenye ulemavu au wenye mahitaji maalum. Hii ni katika utekelezaji wa Mikataba na Maazimio mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa na Ilani Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025.

Aina ya Ushirika utakaoanzishwa na Wanawake wa Mkoa wa Geita utatumia uzoefu wa mafanikio yaliyopatikana kwenye Ushirika wa Madirisha Women Cooperative Society uliopo Mkoani Dar Es Salaam ili kuwafikia na kuwaunganisha wanawake wote wa Mkoa wa Geita kwa kila Wilaya ambao ni wazalishaji ili kuweza kumiliki na kushiriki katika uchumi jumuishi.

Ushiriki wa Wanawake kwenye uchumi wa viwanda umekuwa mdogo sana kutohana na sababu mbalimbali za Kiuchumi kama vile ukosefu wa mitaji, uzalishaji mdogo, biashara isiyendelevu, ukosefu wa Masoko ya mazao na bidhaa zinazozalishwa na sababu zingine za kijamii kama vile elimu duni, masuala ya kifamilia na utamaduni.

Ushiriki wa Wanawake kuitia muundo wa MADIRISHA utasaidia kuwaunganisha Wanawake, kufikia mahitaji mapya ya sekta binafsi, kuongeza tija na uongezaji thamani ya mazao na bidhaa za Wanawake wajasiriamali, kuongeza ajira kwa vijana na wanawake, kuwa na soko la uhakika la bidhaa na mazao yanayozalishwa katika maeneo husika.

Mkutano huo wa Uhamasishaji wa uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya Wanawake Mkoa wa Geita umehudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Geita, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Geita, Makatibu Tawala, Wakuu wa idara, Mrajis wa Vyama vya Ushirika, na Mwakilishi toka MADIRISHA WOMEN COOPERATIVE SOCIETY ya Mkoani Dar Es Salaam, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ushirika, na Wanawake wajasiriamali wapatao 165 kwa lengo la kuhimiza uanzishaji wa Ushirika huo.

## WAJUMBE WA BODI MKOANI TABORA WAPATIWA MAFUNZO YA USIMAMIZI WA VYAMA

Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika Mkoani Tabora wameanza kupatiwa Mafunzo ya Usimamizi wa Vyama hivyo. Mafunzo yalianza kutolewa Wilayani Urambo kuanzia tarehe 09 hadi 10/05/2022; na Mafunzo yaliendelea kutolewa Wilayani Kaliua kuanzia tarehe 11 hadi 12/05/2022, Sikonge kuanzia tarehe 13 hadi 14/02/2022, Uyui 16 hadi 17/05/2022 na mwisho Tabora Manispaa kuanzia tarehe 18 hadi 19/05/2022.



Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika Mkoani Tabora (Urambo) wakiwa katika mafunzo

Mafunzo hayo yалиhusu Dhana ya Ushirika; Uongozi, Utawala Bora na Maadili ya Ushirika; Uendeshaji na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika; Uwasilishaji wa Hesabu na Ukaguzi; Elimu ya Kodi; na Elimu ya masuala ya Rushwa.

## WAANDISHI WASHINDA TUZO ZA UANDISHI WA HABARI ZA USHIRIKA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Mjaliwa, akiwa Mgeni Rasmi katika utoaji Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), 2021 alikabidhi Tuzo mshindi wa jumla pamoja na mshindi wa Tuzo ya Maisha ya Mafanikio Katika Uandishi wa Habari.



Tuzo hizo zimetolewa Mei 28, 2022 katika ukumbi wa Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam ambapo mshindi wa Tuzo ya Maisha ya Mafanikio Katika Uandishi wa Habari ni Ndimara Tegambwage.

Washindi wa Tuzo za Uandishi wa Habari za Ushirika ni Baraka Messa, Mwandishi wa gazeti la Habari Leo aliyeandika kuhusu Wanawake wa Mbozi Mkoani Songwe Walivyopaza Sauti ili Kuongezwa kwa Bajeti ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Ushirika; na Martha Nalimi, aliyeandika na kutangaza kwenye Redio kuhusu Umuhimu wa Kujunga na Vyama vya Ushirika Nchini.



Mwenyekiti wa Tuzo hizo, Kajubi Mkajanga mesema kuwa idadi ya wateule wa EJAT 2021 kwa upande wa wanawake ni 28 ambayo ni sawa na asilimia 47, ikiwa ni ongezeko la asilimia tatu ukilinganisha tuzo zilizopita ambapo wanawake walikuwa ni 26 sawa na asilimia 44 walioingia kwenye hatua hii kwa mwaka jana. Na wateule wanaume ni 32 sawa na asilimia 53.

Aidha, Pamoja na Tuzo za umahiri wa uandishi wa habari Tanzania (EJAT), Washindi wa Tuzo za Uandishi wa Habari za Ushirika; Baraka Messa, Mwandishi wa gazeti la Habari Leo, Martha Nalimi, aliyeandika na kutangaza kwenye Redio, pamoja na Lugenzi Kabale wa TBC walikabidhiwa pia zawadi katika Maadhimisho ya SUD kwa mwaka 2022 yaliyofanyika kitaifa mkoani Tabora.



## MAAFISA USHIRIKA WAKABIDHIWA PIKIPIKI KUTOKA TCDC

Maafisa Ushirika katika Mikoa mbalimbali nchini wamekabidhiwa pikipiki kwa ajili ya kurahisisha utendaji wa majukumu katika kuhudumia Wanaushirika kwenye Mikoa hiyo. Pikipiki hizo zimenunuliwa na Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliyo chini ya Wizara ya Kilimo ikiwa ni mahususi kwa ajili ya usimamizi shughuli za Vyama vya Ushirika.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Sophia Mjema, akikabidhi pikipiki) kwa Maafisa Ushirika wa Mkoa huo



Aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzore, akikabidhi Pikipiki kwa Maafisa Ushirika wa Wilaya za Misenyi, Muleba na Bukoba DC.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro (sasa RC Geita), Mhe. Martine Shigela, akikabidhi pikipiki) kwa Maafisa Ushirika wa Mkoa huo

## NAIBU WAZIRI WA KILIMO AWATAKA WASIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA KUIMARISHA MIFUMO YA USIMAMIZI

Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Anthony Mavunde, amewataka Wasimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Vyama ili kusimamia mali na fedha za Wanaushirika kwa lengo la kuwawezesha Wanachama kunufaika na Huduma zinazotolewa katika Vyama hivyo.

Naibu Waziri ametoa wito huo wakati akifungua Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) yaliyoanza tarehe 28 Juni, 2022 Mjini Tabora ambapo Wanaushirika nchini kote walikutana kwa lengo la kutathmini mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika Sekta ya Ushirika nchini.



*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Anthony Mavunde, (wa tatu kulia) akifuatilia ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD - 2022), mjini Tabora.*

Naibu Waziri Mavunde ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendelea kuimarisha Mfumo wa Kanzidata na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika na Wanaushirika nchini, kusimamia na kuratibu kwa ukaribu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika.

Aidha. Mhe. Mavunde amelielekeza Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), kuendelea kuimarisha Mifumo ya Udhibiti na Usimamizi wa mali zikiwemo fedha ya Vyama vya Ushirika.

Mhe. Mavunde amekitaka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kuendelea kutoa elimu ya Ushirika kwakuwa wananchi wengi na Wadau hawajajua Ushirika na umuhimu wa kujiunga na Vyama vya Ushirika.

Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) limetakiwa kuhakikisha kuwa linatoa huduma kwa Vyama vya Ushirika ikiwemo mafunzo, masoko, utafiti na ushauri wa namna bora ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika.

## WANAWAKE WATAKIWA KUJIUNGA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian, amewataka Wanawake nchini kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili kuwawezesha kupata Mitaji na kuanzisha biashara mbalimbali ikiwemo Viwanda vitakavyomilikiwa na Wanaushirika wenyewe.



*Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian, akizungumza katika siku ya pili ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD), mjini Tabora*

Mkuu wa mkoa wa Tabora ametoa wito huo, tarehe 29 Juni 2022 katika siku ya pili ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) yaliyofanyika Kitaifa Mjini Tabora. Balozi Dkt. Burian amesema wanawake watakapojiunga katika Vyama vya Ushirika itawawezesha kupata Nguvu ya pamoja ya kiuchumi na hivyo kuchangia kwenye kuinua pato la familia na la Taifa kwa ujumla.

"Wanawake tuijungeni katika Vyama vya Ushirika bila kujali vyeo au Madaraka tuliyonayo; mimi ni mwanachama wa Chama cha Ushirika cha Arusha Women's Business SACCOS (AWIB) na kuna wanajeshi wa vyeo mbalimbali na viongozi wa ngazi tofauti wamejiunga katika ushirika hivyo kina mama wenzangu tuitumie fursa iliyoko katika Ushirika kujiletea maendeleo," amesema Dkt. Burian.



*Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian, akitembelea mabanda ya Wanaushirika kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD), mjini Tabora*

Naye Mrjis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt Benson Ndiele, amesema Serikali kuititia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imedhamiria kuwawezesha Watanzania walio wengi kuijunga na Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi na kutumia fursa zinazopatikana katika Sekta mbalimbali.

## KONGAMANO LA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA LAFANYIKA TABORA

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe tarehe 30 Juni, 2022 alifungua Kongamano la Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, liliolofanyika Mjini Tabora kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) mwaka 2022.

Mhe. Naibu Waziri amewapongeza Wanaushirika kwa kuendelea kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika kuuza kwa pamoja kuititia minada na utafutaji masoko ili kupata bei nzuri za mazao yao.

Mhe. Kigahe ameyataja Mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ni pamoja na ongezeko la bei za mazao, mapato ya mkulima na Mapato ya Serikali kwa wastani wa asilimia 200; na ongezeko la uzalishaji wa mazao kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka.



*Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe, akifungua Kongamano la Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, liliolofanyika Mjini Tabora*

Mafanikio mengine ni Mfumo ni kuwa kichocheo cha Ubora wa mazao yanayofikishwa sokoni; upatikanaji wa takwimu sahihi za mazao; kukuza huduma za fedha vijijini na kufanikisha Uanzishwaji wa Soko la Bidhaa Tanzania.

Mfano wa manufaa ya bei ni zao la Choroko kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuongezeka kwa asilimia 25, zao la Kakao kuongezeka kwa asilimia 250 na bei ya zao la Korosho kuongezeka kwa asilimia 168 ikilinganishwa na bei wakati wa Mfumo holela wa mauzo ya mazao hayo.

Akizungumza katika Kongamano hilo Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amewataka Wanaushirika kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kuwawezesha Wanaushirika Kuongeza thamani ya mazao ya wakulima na kukuza kipato chao.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Stakabadhi za Ghala, Asangye Bangu, amesema Bodi hiyo iliyozanzishwa mwaka 2007/2008 katika zao la Korosho imeendelea kupanuka katika mazao mbalimbali ikiwemo Ufuta, Kakao, Kahawa, nafaka na mazao jamii ya Kunde.

Bangu amesema hadi kufikia mwaka 2021/2022, Bodi imesimamia ukusanyaji wa mazao kupitia Mfumo zaidi ya Kilogramu billioni 2.3, na kuleta utulivu wa mtiririko wa Bidhaa kutoka shambani hadi sokoni ikilinganishwa na mazao yanayouzwa kupitia mifumo isiyo Rasmi.

## MCHAKATO WA UANZISHWAJI BENKI YA USHIRIKA UFANYIKE MAPEMA - DKT. ISHENGOMA

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Ufugaji na Maji, Mhe. Dkt. Christine Ishengoma amesema; ili kuongeza tija kwenye Ushirika ni vyema mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ukafanyika mapema iwezekanavyo kwa kuwa wazo la kuanzisha Benki ya Ushirika ni la Wanaushirika wenywewe, hivyo hii inafanya mchakato wake kuwa rahisi.

Dkt. Ishengoma ameyasema hayo alipokuwa akifunga Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani lililofanyika tarehe 1 Julai 2022 Mjini Tabora.

"Kwakuwa Serikali imeonyesha nia njema ya kuhakikisha adhma hii ya uanzishaji wa Benki ya Kitaifa ya Ushirika inakamilika; napenda kutoa wito wangu kwenu Wanaushirika, kununua Hisa katika Benki hii ya Ushirika," amesema.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Ufugaji na Maji, Mhe. Dkt. Christine Ishengoma, akifunga Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani - 2022*

"Katika kongamano la Siku ya Ushirika Duniani mmejadili mambo mbalimbali ikiwemo Mifumo ya Kodi, Stakabadhi Ghalani, matumizi ya TEHAMA na Mifumo ya Masoko, na Huduma za Fedha pamoja na changamoto nyingi zinazowabili Wanaushirika; lengo kuu la mijadala hii ni kuona jinsi ambavyo Ushirika unaweza kusaidia kujenga limwengu Bora," amesema Dkt. Ishengoma.

Akizungumza katika Kongamano hilo, Mrasis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkoo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndyege, amesema kwa sasa Serikali imejikita katika kuendesha Vyama vya Ushirikai katika Mifumo ya kidijitali ili kuendana na kasi itakayoviwezesha vyama kupiga hatua kwa haraka.

Aidha, Dkt. Ndyege amewakumbusha Wanaushirika kuendelea kununua Hisa katika Benki ya Ushirika Kilimanjaro ili kufanikisha lengo la kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika.

Amevitaka Vyama vya Ushirika kuendelea kujenga Maghala katika Vyama vyao ili kuwezesha na kurahisisha uuzwaji wa mazao, na kujenga viwanda vya kuchakata mazao na kuongeza kasi ya ukuwaji wa Sekta ya Kilimo.

Akizungumza katika Kongamano hilo, Kuelekea Siku ya SENSA mwezi Agosti 2022, Kamishna wa SENSA na Spika Mstaafu, Mhe. Anna Makinda, amewahimiza Wanaushirika kushiriki kikamilifu katika zoezi Sensa ili kusaidia Serikali kujua Idadi ya watu wake ili kuwezesha kupanga Bajeti ya Taifa kwa usahihi.

## TUME YA USHIRIKA NA BENKI YA NMB ZAINGIA MAKUBALIANO UJENZI WA MAGHALA KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeingia Randama ya Makubaliano na Benki ya NMB kushirikiana katika kuwezesha ujenzi wa maghala kwenye Vyama vya Ushirika nchini.



*Mrasis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkoo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndyege, na Kaimu Afisa Mtendaji Mkoo wa Benki ya NMB, Juma Kimori wakionesha Mkataba wa Makubaliano*

Makubaliano haya yametiwa saini Jijini Dodoma tarehe 15/06/2022 kati ya Mrasis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkoo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndyege, na Kaimu Afisa Mtendaji Mkoo wa Benki ya NMB, Juma Kimori ambapo wamesema ushirikiano huo una lengo la kuhakikisha maghala yanajengwa kwenye Vyama vya Ushirika nchi nzima. Benki ya NMB imetenga Bilioni 20 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa maghala kwenye Vyama vya Ushirika.

"Matarajio tuliyonayo ni kutatua changamoto ya kukosekana kwa maghala yenye ubora katika Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama

Vikuu kwa mazao ya Kimkakati na maghala haya yatatumika pia kwenye mazao mengine yanayolimwa na wakulima katika maneo yao," amesema Dkt. Ndieu.



Picha ya pamoja mara baada ya kutia saini Randama ya Makubaliano kati ya TCDC na NMB

Aidha, Mrajis ametoa wito kwa Vyama vya Ushirika: kushirikiana na benki ya NMB na TCDC katika kutoa taarifa za uzalishaji ili kubaini ukubwa wa ghala unaohitajika; kushirikiana kwa Benki ya NMB na TCDC katika utekelezaji wa shughuli za Randama ya Makubaliano ili kufanikisha ujenzi wa Ghala; na Kutunza maghala yatakayojengwa au kuboreshwa kupitia makubaliano yaliyofikiwa.



Mtendaji Mkoo wa FSDT, Pamela Shao na Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndieu, wakibadilishana Mkataba wa Makubaliano kati ya TCDC na FSDT

Akizungumza katika hafla hiyo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndieu amesema maeneo yatakayotekelezwa kupitia mkataba huo wa makubaliano ni kuimarisha utekelezaji wa Sera na miongoz mbalimbali katika shughuli za Vyama vya Ushirika; kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa kuhakikisha vinapata watendaji wenye sifa wanaoweza kufanya kazi kwa ajira za muda wa kati na muda mrefu; na kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa Vyama vya Ushirika.

## TCDC NA FSDT ZAINGIA MAKUBALIANO KUIMARISHA VYAMA VYA USHIRIKA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT) zimetia Saini Randama ya Makubaliano kufanya kazi pamoja katika maeneo ya Utafiti na shughuli zingine zinazolenga kuwainua Wanaushirika.

Makubaliano hayo yametiwa saini tarehe 21 Juni 2022 Jijini Dodoma na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkoo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndieu na Mtendaji Mkoo wa FSDT, Pamela Shao.

Masuala mengine yatakayoshughulikiwa kupitia Ushirikiano huo ni pamoja na Elimu na Mafunzo kwa Wanachama na Watendaji wa Vyama vya Ushirika; na kutekeleza vipaumbele vilivyoko katika Mpango Mkoo wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha kwa miaka kumi na Agenda ya 10/30 ya mwaka 2022.



Picha ya Pamoja mara baada ya kutia saini Randama ya Makubaliano kati ya TCDC na FSDT

Mtendaji Mkoo wa FSDT, Pamela Shao, amesema katika kutekeleza makubaliano hayo Mikoa 15 itahusika kwenye miradi itakayopangwa na itaanzia katika Mkoa wa Morogoro Wilayani Kilombero kwa Wakulima wa Miwa.

TCDC katika utekelezaji wa majukumu yake ya Udhibiti na Uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika nchini, imekuwa ikishirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo kwa lengo la kuwasaidia Wananchi hasa Wakulima wadogo kuweza kushiriki katika shughuli zao za uzalishaji, Uongezaji thamani wa mazao, Masoko na Uwekezaji.

## VIONGOZI WA USHIRIKA WATAKIWA KUWA WAAMINIFU NA MADHUBUTI

Viongozi wa Vyama vya Ushirika wametakiwa kuwa Waaminifu na Madhubuti wanapovisimamia na kuviendesha Vyama hivyo kwaniaba wanachama.

Wito huo umetolewa na James Mchembe, Katibu Tawala wa Wilaya ya Arumeru, kwa niaba ya Mkoo wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, kwenye Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika Mkoa wa Arusha, 18 Juni, 2022.



“Tukiweza kuwa na Viongozi madhubuti itasaidia zaidi hata Serikali yetu isiwe inasumbuka katika usimamizi wa Vyama hivi; chama kikiwa vizuri basi kila mmoja wetu atakuwa vizuri,” alisema Mchembe.

Akisoma Risala kwa niaba ya wanachama wenzake katika Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika Mkoa wa Arusha, Meneja wa Kanono SACCOS na Mwenyekiti wa Jukwaa, Wilbard Ngambeki, amesema Wanaushirika wanaomba kurudishiwa Maghala yaliyochukuliwa na Serikali za vijiji kipindi vyama vya Ushirika vilipofutwa kwakuwa serikali za vijiji haviyatumii Maghala hayo zaidi ya kukodisha.

Katika tukio jingine, Mwakilishi wa Mkoo wa Mkoa wa Arusha, Mchembe amekabidhi Pikipiki tatu kwa Maafisa Ushirika wa Mkoa huo, ambazo zimenunuliwa na Serikali kuitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) mahususi kwa ajili ya kuwasaidia Maafisa Ushirika katika usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

## VYAMA VYA USHIRIKA DAR-ES-SALAAM VYAOMBA KUPUNGUZIWA KODI YA MAPATO

Vyama vya Ushirika Mkoani Dar es salaam vimeiomba Serikali kuitia Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kuvipunguzia Vyama hivyo Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 hadi kufikia asilimia 10. Ombi hilo limetolewa tarehe 9 Juni, 2022 katika Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dar es salaam.



Viongozi wa Ushirika Mkoani Dar es Salaam wakiwa na Mgeni Rasmi, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha, Josephat Kisamalala (wa tatu kushoto)

Mgeni Rasmi katika Kongamano hilo alikuwa Mrajis wa Vyama Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ambae aliwakilishwa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha, Josephat Kisamalala, alisema amepokea maoni hayo na kwakuwa yako chini ya Mamlaka ya Mapato (TRA) watayafutilia. Aidha, amesisitiza suala la Waajiri kuweka fedha kwa wakati za makato ya fedha za wafanyakazi ambao wapo kwenye Vyama vya Ushirika.

Mrajis Msaidiz wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Dar es salaam, Abdilahi Mutabazi amewataka wanachama wa Vyama vya Ushirika kufanya mapinduzi ya kiuchumi. "Tuna chama chetu Cha DASIKO LTD wameshaagizia machine kwa ajili ya kutengenezea bati niwasihii Vyama vya Ushirika, kama kununua samani za maofisi twende tununue DASIKO LTD," alisema Mutabazi.

Wanaushirika Mkoani Dar es Salaam wakiwa na Mgeni Rasmi, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha, Josephat Kisamalala (wa tatu kushoto waliokaa)

### ➤ Wachaguliwa Kuongoza Jukwaa la Ushirika Dar es Salaam

Jukwaa la Ushirika mkoa wa Dar es Salaam Jana tarehe 10 Juni, 2022 limechagua Viongozi wapya baada ya Viongozi waliokuwepo kumaliza muda wao wa miaka miwili wa kuwepo madarakani.

Katika Uchaguzi huo, Musa Chowo alichaguliwa kuwa mwenyekiti mpya wa Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Emaculata Joctan aliyechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa jukwaa hilo.



Viongozi wapya wa jukwaa la ushirika mkoa wa Dar es salaam wakitambulishwa na Mrajis msaidizi wa vyama vya ushirika mkoa wa Dar es salaam Abdilahi Mutabazi (wa kwanza kushoto)

## **SERIKALI YAKIKABIDHI KIWANDA CHA MANONGA GINNERY KWA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA IGEMBENSABO**

Serikali imelazimika kumnyang'anya Mwekezaji kiwanda cha kuchambua Pamba cha Manonga Ginnery kilichopo Wilayani Igunga Mkoani Tabora kutokana na Mwekezaji huyo Rajan Metal Machinery kushindwa kukiedeleza baada ya kuonekana amekitelekeza huku akizifungua baadhi ya mashine na kuzihamisha ndani ya majengo ya kiwanda hicho.

Hatua hii ya ya makabidhiano imefanyika siku ya Jumatatu, Juni 13, 2022 kufuatia Serikali kufanya mazungumzo ya mara kadhaa na mwekezaji huyo ambaye alionekana kutokuwa na nia ya kukiedeleza kiwanda hicho ambacho kina umiliki wa asilimia 80 huku asilimia 20 ikimilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika Igembensabo.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dkt. Batilda Burian, akiwa ameambatana na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, alifika katika kiwanda cha Manonga na kutaka kujuu ni vipi mashine zimefunguliwa

na kuhamishwa; na baada ya kukosa majibu ya kuridhisha aliamua kukabidhi kiwanda hicho kwa Chama Kikuu cha Ushirika Igembensabo.

Baadhi ya wafanyakazi waliokitumikia kiwanda cha Manonga nao bado wako na kilio cha madai ya haki zao huku kiwanda kikiwa kimesalia na mitambo isiyofanyakazi na ni vyuma chakavu. Kutokufanyakazi kwa kiwanda hiki ni dhahiri kilikuwa chanzo cha kuzorota kwa sekta ya Kilimo cha pamba Mkoani Tabora.



*Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dkt. Batilda Burian, akikabidhi funguo za kiwanda kwa viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika Igembensabo.*

## **TCDC KATIKA MEI MOSI - 2022**

Wafanyakazi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Mei 01, 2022 wameshiriki Maadhisho ya Sikukuu ya MEI MOSI Kitaifa Jijini Dodoma, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



## JIFUNZE KUTOKA CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO USALAMA WA RAIA (URA SACCOS)

### 1. Historia Fupi ya Chama

URA SACCOS LTD ni Chama cha kuweka Akiba na Mikopo kilichoanzishwa kwa ajili ya kuwahudumia watumishi wa Jeshi la Polisi Tanzania pamoja na Familia zao. Chama hiki kilisajiliwa mnano tarehe 06 Septemba, 2006 chini ya Sheria ya ushirika Na.20 ya mwaka 2003 na kupata namba ya usajili DSR 904. Chama pia kimepata leseni Na. MSP3-TCDC/2021/00103 chini ya sheria inayosimamia sekta ya huduma ndogo ya fedha ya mwaka 2018.

Fungamanisho la chama linaundwa na watumishi wa jeshi la Polisi Tanzania (Askari Polisi, watumishi raia katika Idara ya Polisi) pamoja na familia zao ambao ni wenza na watoto, kikiwa na dira ya kuwa taasisi ya kifedha iliyo imara kifedha, endelevu na yenye mtandao mpana kitaifa inayohudumia fungamanisho lake kwa dhamira ya kutoa huduma bora yenye gharama na masharti nafuu yanayokidhi mahitaji ya wanachama.


Chama hiki kilizinduliwa na aliyekuwa Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya M. Kikwete mnano tarehe 09 Septemba, 2006 katika ukumbi wa Diamond Jubilee Dar es salaam.



### 2.0 Hali ya Uanachama na Muundo wa Uongozi

Chama kina wanachama 41,766 kwa sasa ukilinganisha na wanachama 4,300 kwa mwaka 2006 wakati Chama kinaanzishwa. Ongezeko hili ni zaidi ya 971%.

### MUUNDO WA UONGOZI ULIOPO



## 2.1 Mkutano Mkuu

Mkutano mkuu unaweza ukawa; (Mkutano mkuu wa mwaka, Mkutano mkuu wa kawaida ama Mkutano mkuu maalum). Hiki ndicho chombo kikuu cha maamuzi, kuongoza na kusimamia shughuli zote katika chama, kinaundwa na wanachama wote kwa uwakilishi wa mjumbi mmoja kutoka katika kila Kikosi cha Polisi, Mkoa, Makao Makuu ya Polisi na Wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

## 2.2 Bodi ya Chama

Hiki ndicho chombo kinachobeba dhamana kisheria kusimamia shughuli zote za kila siku na kutunza fedha na mali zote za Chama, kinaundwa na wajumbe tisa wanaochaguliwa na Mkutano mkuu.

## 2.3 Kamati ya Usimamizi

Kamati hii inaundwa na wajumbe watatu wanaochaguliwa na Mkutano mkuu, jukumu lao ni kuhakikisha kuwa taratibu zote za uendeshaji wa Chama zinafuatwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, masharti ya chama, sera za chama na miongozo mbalimbali inayosimamia Vyama vya ushirika vinafuatwa.



## 2.4 Kamati ya Mikopo

Kamati hii ina wajumbe watatu ambao ni sehemu ya wajumbe wa Bodi waliochaguliwa mionganii mwao, ikiwa na jukumu la kusimamia utaratibu wa utoaji, ufuutiliaji na ufutaji wa mikopo kwa kuzingatia Sera ya Mikopo ya Chama.

## 2.5 Meneja Mkuu

Meneja Mkuu ana wajibu wa kusimamia utekelezwaji wa shughuli zote za kila siku za chama kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 27 ya Huduma Ndogo za Fedha pamoja na Masharti ya chama sehemu ya kumi.

## 2.6 Idara Mbalimbali

Idara ya Uhasibu: Inahusika na shughuli zote za uaandaji wa taarifa zote za kifedha za Chama  
Idara ya Mikopo: Inahusika na shughuli zote za uandaaji na utoaji wa mikopo kwa wanachama  
Idara ya masoko na elimu: Inahusika na shughuli zote za utoaji wa elimu kwa wanachama na utangazaji wa Chama  
Idara ya Tehama: Inahusika na shughuli za kielektroniki za Chama  
Idara ya Uhusiano: Inahusika na shughuli zote za huduma kwa mteja

## 2.7 Matawi

Chama kina matawi ambayo yataanza kufanya kazi chini ya usimamizi wa URA SACCOS Makao Makuu, ili kuweza kurahisisha huduma katika maeneo na kanda husika kwa ukaribu zaidi, matawi haya ni: Dar es salaam, Mbeya, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Zanzibar na Tanga.

## 3. Miongozo na Sera Zilizopo

Chama kimetengeneza miongozo mbalimbali ili kurahisisha na kusaidia muundo na mfumo katika ufanyaji kazi wake ikiwemo:

- (a) Masharti ya chama.
- (b) Mpango mkakati.
- (c) Mpango biashara.
- (d) Sera ya uhamasishaji wa kuweka akiba, hisa na amana.
- (e) Sera ya ununuzi.
- (f) Sera ya menejimenti ya ukwasi na dhima.
- (g) Sera ya Rasilimali watu.
- (h) Sera ya udhibiti wa ndani.
- (i) Sera ya udhibiti wa vihatarishi na majanga.
- (j) Sera ya uhaisbu na fedha.
- (k) Sera ya ulinzi wa mlaji.
- (l) Sera ya utoaji, ukusanyaji na ufutaji mikopo.

#### 4. Dhana ya Utawala na Uongozi Bora

Kwa kusimamia na kutekeleza dhana nzima ya utawala bora, chama kimekuwa kikisimamia katika kuhakikisha ujumuishaji na ushirikishwaji wa wanachama wote katika maamuzi na utekelezaji wa maamuzi yanayohusu mustakabali na maendeleo yao na chama chao. Haya yanafanya kwa kuzingatia misingi ifuatayo:

**Demokrasia:** kwa kuzingatia hili chama tokea kuanzishwa kwake kimekuwa kikipata viongozi wake kwa njia ya uchaguzi huru ambao husimamiwa na Tume ya maendeleo ya Ushirika kwa kupitia warajis na Maafisa ushirika wake na hakujawahi kutokea mgogoro wa aina yoyote wa kiuongozi tokea chama kuanzishwa mwaka 2006. Pia katika mikutano mbalimbali ya chama:

- (a) kumekuwa na kuvumiliana kwa staha kwa mitizamo na maoni tofauti;
- (b) Kufuata na kuheshimu mawazo ya walio wengi;
- (c) Kutumia nguvu ya hoja na siyo hoja ya nguvu;
- (d) Kupingana bila kupigana; na
- (e) Kujikosoa na kukosoana bila kuoneana

**Uwazi:** chama kimekuwa kikitoa taarifa mbalimbali kama vile za kifedha na mwenendo mzima wa chama kwa wanachama wake bila kificho kikitumia njia mbalimbali ikiwemo kuzichapisha taarifa hizo na kuzigawa kwa wanachama na wakati mwagine kuziweka hadharani katika matamasha na maonesho mbalimbali ya kiushirika.

**Utawala wa Sheria:** Chama kimekuwa kikifuata sheria, kanuni na taratibu zote zinazosimamia ushirika na kimetengeneza masharti na sera mbali mbali zinazokiongoza.

**Ushirikishwaji wa wanachama:** chama kimekuwa kikiitisha mikutano na utoaji wa elimu kila mara na kupokea mawazo na ushauri mbalimbali kutoka kwa wanachama wake

#### 5. Viashiria Vinavyoonyesha Jinsi URA SACCO Ilivyofuata Misingi ya Ushirika

##### **Kanuni ya 1: Wanachama ulio wazi**

Wanachama wamekuwa wakiongezeka kwa hiari yao toka wanachama 4,300 mwaka 2006 hadi wanachama 41,766 mwaka 2021. Huduma za chama zimekuwa zikitumiwa na wanachama kwa mfano hisa zimenunuliwa hadi kufikia thamani ya Shilingi 8,206,081,104/= mwaka 2020 ukilinganisha na hisa zenye thamani ya Shilingi 17,026,693/= mwaka 2006, akiba za wanachama zimefika Shilingi 62,879,650,292/= ukilinganisha na Shilingi 76,748,917/= mwaka 2006, mikopo imefika Shilingi 282,693,053,038 ukilinganisha na mikopo yenye thamani ya Shilingi 3,938,636,500 mwaka 2007.

##### **Kanuni ya 2: Uongozi wa kidemokrasia**

Kutokuwa na mgogoro wowote wa kiuongozi tokea kuanzishwa kwa chama.

##### **Kanuni ya 3: Kushiriki kwa wanachama kiuchumi**

Wanachama wote wamekamilisha kulipia hisa zao pia wanachangia akiba kulingana na taratibu zilizopo na kutumia huduma ya mikopo bila malalamiko.

##### **Kanuni ya 4. Chama cha ushirika ni chombo huru**

Chama kimekuwa kikifanya maamuzi yake bila kuingiliwa kwa maslahi ya wanachama wake.

##### **Kanuni ya 5: Mafunzo, elimu na habari**

Chama hufanya mafunzo na kutoa elimu kwa wanachama kwa kuzingatia mpango kazi wake wa kila mwaka. Pia chama huchapisha vipeperushi vya kuhabarisha na kutoa matangazo mbalimbali na kuyasambaza kwa wanachama wake.

##### **Kanuni ya 6: Ushirikiano baina ya Vyama vya Ushirika**

Chama kimekuwa kikishiriki katika maadhisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD) na makongamano ya kiushirika kwa kuungana na vyama vingine, pia kutembelea na hata kutembelewa na

vyama vingine kwa minajili ya kujifunza mambo mbalimbali.

#### **Kanuni ya 7: Ushirika kujali jamii**

Chama kimekuwa kikitoa misaada mbalimbali katika jamii inayokizunguka, kwa mfano, Chama kimeishatoa msaada ya vifaa tiba katika hospitali na zahanati za Polisi nchini vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi 250,000,000/=

#### **6. Mafanikio kwa Ujumla**

Chama kimekuwa kikishuhudia mafanikio makubwa tokea kuanzishwa kwake hadi hivi sasa kama vile ongezeko la wanachama, akiba, hisa na utumiaji wa mikopo. Pia rasilimali na dhima za Chama kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo vimekuwa vikiongezeka.

#### **Wanachama**

Chama kilianzishwa na wanachama wapatao 4,300 mwaka 2006 na hadi kufikia sasa kimekuwa na ongezeko la wanachama kufikia 41,766 mwaka 2020.

#### **Hisa**

Hisa zenye thamani ya Shilingi 17,026,693/= kwa mwaka 2006 zimeongezeka hadi kufikia Shilingi 8,206,081,104/= kwa sasa.

#### **Akiba**

Hisa zenye thamani ya Shilingi 76,748,917/= kwa mwaka 2006 zimeongezeka hadi kufikia Shilingi 62,879,650,292/= kwa sasa.

#### **Utoaji Mikopo**

Mikopo yenye thamani ya Shilingi 3,938,636,500/= kwa mwaka 2007 imeongezeka hadi kufikia Shilingi 282,693,053,038/= kwa sasa.

#### **7. Mahusiano na Asasi Nyingine**

Chama kimeendelea kuwa na uhusiano mzuri baina yake na vyama vingine mbalimbali kwa kupokea mawazo na ushauri mbalimbali kuhusu uendeshaji wa ushirika, na kutembelea vyama vingine ili kujifunza kwa vitendo, vile vile, chama kimekuwa kikitoa ushauri na mawazo mbalimbali kwa vyama vingine sambamba na kutembelewa na vyama vingine kwa minajili ya kujifunza. Pia, mbali na Chama kuwa mwanachama wa SCCULT kimekuwa na ushirikiano mzuri na menejimenti yake kwa kufuata maelekezo na miongozo yote inayotolewa na mabenki, taasisi mbalimbali za serikali ikiwemo Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo ni msimamizi na mwangalizi wa jinsi sheria ya ushirika na kanuni zinavyoteklezwa.

**Jedwali Na 1: Wadau wa chama na manufaa yake**

Jina la taasisi	Aina ya taasisi	Maeneo/nyanja za ushirikiano	Matokeo ya ushirikiano
Shirikisho la Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT)	Shirikisho la vyama vya ushirika vya akiba na mikopo la kitaifa/chama kilele	(a) Mafunzo na ushauri kwa viongozi na watendaji (b) Kuandaa na kushiriki katika siku ya vyama vya ushirika wa akiba na mikopo inayofanyika kila mwaka	Ongezeko la uelewa na ufanisi kwa viongozi na watendaji
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)	Taasisi ya serikali ya kusimamia maendeleo ya ushirika	a) Kutoa maelekezo kuhusu sera na sheria ya ushirika b) Kushirikishana mbinu za kuendesha vyama vya ushirika kwa ufanisi c) Kubadilishana taarifa na takwimu kuhusu vyama vya ushirika d) Kuandaa na kufanya majukwaa ya ushirika e) Kutangaza mafanikio na visa mafunzo vya ushirika	a) Chama kufahamika ngazi ya mkoa na taifa b) Ongezeko la wageni kujifunza ufanisi wa Chama
Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika, Dodoma (COASCO)	Shirika la Serikali la Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika	Kufanya ukaguzi wa hesabu za chama	Chama kukaguliwa hesabu na kupata fursa ya kujirekebisha hasa kwenye dosari zinazobainishwa na mkaguzi

**8. Hitimisho**

Mabadiliko ya teknonolojia na kukua kwa chama – kiuwanachama, mtaji na huduma za kibiashara kwa wateja, ni mambo ya msingi kuzingatia katika kuboresha mbinu za kiuongozi. Uchambuzi wa mara kwa mara wa kitaasisi umeendelea kuisadia URA SACCOS kuchukua hatua zitazosaidia uongozi kuendana na mazingira na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kwa mfano namna ya kuhakikisha wanachama wanapata bidhaa na huduma zinazokidhi mahitaji yao.

## **UJUMBE WA USHIRIKA KIPITIA VIBONZO (KATUNI)**





TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA



## USHIRIKA NI FURSA



*Limetolewa na*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA.

Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973

B.Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: [www.ushirika.go.tz](http://www.ushirika.go.tz)

ushirika\_tcdc Tume ya Maendeleo ya Ushirika